For more visit: eazyarabic.com

# KCSE 2013 Paper 2

## 4.2.2 Kiswahili Paper 2 (102/2)

**1. Ufahamu**

(a) (i) Kuharibika kwa miundomsingi/barabara mbovu
(ii) Mishahara duni
(iii) Malalamishi yao kutosikilizwa
(iv) Kutothaminiwa kwa utaalamu
(v) Kukosa huduma za kimsingi k.v. maji
(vi) Kuvutiwa na maisha ya kuridhisha huko ng'ambo
(vii) Kutokuwa na matumaini ya mustakabali mwema nchini.

4 x 1 - alama 4

(b) Masika ni hali nzuri au manufaa.
Ng'ambo kuna maisha ya kuridhisha kama vile kuthaminiwa kwa wanataaluma.

1x1 - alama 1

Hata hivyo, kuna dosari zifuatazo:
(i) Upweke
(ii) Ubinafsi
(iii) Baridi

2x1
(Jumla - alama 3)

(c) (i) Umma kutofaidika kutokana na huduma za wataalamu wake licha ya kuwafadhili
(ii) Kuwaachia mzigo wa kazi wataalamu wachache waliobaki
(iii) Kuwapoka riziki wafanyakazi, k.v. walioajiriwa na wataalamu hawa
(iv) Kulazimika kufanya kazi kwa saa nyingi, kama vile Dkt. Tabibu

3 x 1 - alama 3

(d) (i) Huwezesha kuwasiliana na jamaa walio mbali, kwa mfano, Daktari na rafiki yake wanawasiliana kwa simu.
(ii) Huwezesha kuwafikia watoaji huduma patokeapo dharura, kwa mfano Daktari anapigiwa simu nyumbani.
(iii) Hurahisisha usafiri - gari la Daktari.
(iv) Hurahisisha kupata huduma ya karibu ya maji- bomba la maji nyumbani kwa Daktari.

3 x 1 - alama 3

(e) (i) Kuyapa mji - kuyawazia/kuyapa nafasi ya kuyajibu
(ii) Fukuto - wasiwasi/mashaka/dukuduku/kutokuwa na utulivu/hamaniko

2 x 1 - alama 2

2. (a) (i) Katiba mpya iliidhinisha mfumo wa ugatuzi ambao hupunguza mamlaka ya serikali kuu katika usimamizi wa rasilimali.
(ii) Eneo la ugatuzi hutwaa kiasi fulani cha mamlaka.
(iii) Ugatuzi utahakikisha usawa wa kimaendeleo nchini kinyume na awali.
(iv) Serikali isaidie maeneo yote kujiimarisha.
(v) Maeneo yaweke mikakati ya kutafiti na kubainisha rasilimali/zilizomo.
(vi) Kuvumbua rasilimali mwafaka kutasaidia ustawi.
(vii) Wanamaeneo watafute mbinu za kuongezea thamani rasilimali.
(viii) Kilimo cha ufugaji ni nguzo ya maeneo mengi na kinahitaji kuimarishwa kwa kuandama mbinu za kisasa za uzalishaji.
(ix) Ipo haja ya wanaeneo kukabiliana na matatizo yanayohusiana na soko ili kukinga dhidi ya kupoteza wateja.
(x) Ipo haja ya kujenga viwanda vya kuchinjia mifugo na kupakia nyama.
(xi) Baadhi ya wafugaji huhasirika kwa kuuza mifugo wazimawazima.
(xii) Wafugaji wengine hutapeliwa.

7x1=7
Mtiririko = 1
alama - 8

(b) (i) Ujenzi wa viwanda vya kuchinjia na kupakia nyama utakinga dhidi ya kupoteza bidhaa zinazotokana na mifugo.
(ii) Kujenga viwanda hivi kunasababisha ujenzi wa viwanda tegemezi.
(iii) Hili litawezesha kuzalisha nafasi za kazi.
(iv) Kutakuwa na kuongezea thamani utoaji wa huduma za kijamii na kiutawala.
(v) Kuzalisha nafasi za kazi kwa vijana kutasaidia kuwaadilisha vijana zaidi.
(vi) Kila eneo lina vipaumbele tofauti; wakazi wabainishe kipaumbele chao.
(vii) Ugatuzi unahitaji ushirikiano.Kila mwanaeneo awajibikie maendeleo ya eneo.
(viii) Wanaeneo washiriki kuteua viongozi wenye muono mzuri.
(ix) Ufanisi katika maeneo ya ugatuzi utachangia katika ufanisi wa taifa kwa jumla.

6x1=6
Mtiririko = 1
(alama = 7)

3. (a) (i) Sauti mwambatano ni sauti mbili au zaidi zinazotamkwa kama sauti moja (k.v. konsonanti na kiyeyusho. Kwa mfano /tw/

**Au**

Sauti moja ambayo ni muungano wa sauti mbili au zaidi. Kwa mfano konsonanti mbili au tatu. Kwa mfano,/nd/ mb/ ngw/

1 x 2 - (Alama 2)

**Au**

Sauti ambayo huundwa kwa konsonanti mbili au tatu zinazotamkwa kama sauti moja, kwa mfano, /ndw/ katika ndwele,ngw/katika jangwa

(ii) mf: / nd/ - katika unda
/ nz/ - katika mwanzo
/ tw/ - katika twalika
/ nw/ - katika shonwa
/zw/ - katika tuzwa
/sw/ - katika naswa
/ndw/ - katika undwa

1x1 - (Alama 1)

For more visit: eazyarabic.com

Mtahiniwa atumie kielezi cha namna kama ifuatavyo.

(b) Komu ameshona nguo vizuri na kuiuza sokoni
au
Komu aliuza nguo sokoni baada ya kuishona vizuri.
(Alama 2)

(c) (i) Watumie kihusishi cha wakati kama vile, kisha, tangu, halafu, kabla ya, hadi, mpaka, kwa, hata, kufikia, kuanzia. Mfano:
Amekuwa hapa tangu asubuhi.
Aliwasili halafu akaondoka.
(Alama 1)

(ii) Watumie mzizi - o - ote pamoja na nomino / viwakilishi katika ngeli mbalimbali.
Kwa mfano: Mwalimu alitaka kumtuma mtoto yeyote.
Nzi hula kitu chochote.
Hakuweza kula tunda lolote. n.k

(d) Askari wakipiga doria na kushirikiana na raia watakuwa wametuhakikishia usalama.
(Alama 2)

(e)

| a | ta | m | nyw | e | a |
|---|---|---|---|---|---|
| - nafsi, **au**<br>- mtenda, **au**<br>- ngeli, **au**<br>- nafsi ya<br>- tatu, **au**<br>umoja **au**<br>- kiima | - wakati ujao | - mtendewa, **au**<br>- nafsi, **au**<br>- nafsi ya tatu mtendewa, **au**<br>-yambwa tendewa, **au**<br>-yambwa kitondo | mzizi | Kauli **au** tendea<br>Kauli **au**<br>- mnyambuliko | - Kiishio, **au**<br>- Kauli tenda |

$6 \times \frac{1}{2}$ (Alama 3)

(f) Videbe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijundo hivi.
**au**
Vijidebe hivyo vitasafirishwa pamoja na vijijundo hivi.
2x1 - (Alama 2)

(g) (i) Ingawa mshahara wake si mkubwa - tegemezi
(ii) anaikimu familia yake - huru
2x1 (Alama 2)

(h) Matumizi ya 'Kiambishi 'li'
(i) Kiambishi cha wakati uliopita - Musa alitutembelea.
(ii) Kiambishi cha ngeli - Tunda liliiva
(iii) Kiambishi cha kauli tendea - Yule alikukimbilia **au** Mtoto amekalia kigoda.
3 x 1 (Alama 3)

(i) (i) Ni sentensi inayoonyesha kutegemeana kwa matendo au hali.
(Alama 1)

For more visit: eazyarabic.com

(ii) Watumie viambishi na maneno yanayoonyesha kuwa kufanikiwa au kutofanikiwa kwa tukio au tendo moja kunategemea kufanikiwa kwa tukio au tendo lingine. kwa mfano: nge, ngali, ki, kama, iwapo n.k.

(a) Wanafunzi wangefika mapema wangempata mwalimu.
(b) Kotu angalisoma kwa bidii angalifaulu.
(c) Mvua ikinyesha mapema tutapata faida.
(d) Iwapo unataka ufanisi jibidiishe.

**Tanbihi**

Mtahiniwa anaweza kuandika katika hali kanushi kama ville:

(a) Mkulima asingalipanda mapema asingalipata mazao mengi.
(b) Huyu asipojihadhari ataharibikiwa.
(c) Iwapo hutaanza safari mapema utachelewa.
(d) Kama utaanza shughuli mapema hutatatizika.
(e) Lazima asome kwa bidii ili afanikiwe

(Alama 2)

---

(j) (i) La Katunda linapendeza.

**Au**

Tindi anataka cha mwenziwe.

(ii) Atumie viwakilishi vya idadi halisi vinavyotumia a - unganifu. Kwa mfano:

Wa tatu atatuzwa shaba.

**Au**: Mwalimu anamuita wa nne.

1x2 - (Alama 2)

(k) Mifano ifuatayo au zaidi inaweza kujitokeza.

Kairu hajawahi kupalilia mtama.
TS T N

**Au**

Huyu ataweza kukupa ufadhili.
TS T N

**Au**

Wanafunzi hawa wangali wanafanya mtihani.
TS T N

**Au**

Musa alikuwa anawafundisha wanawe.
TS T N

1x2 - (Alama 2)
alama 2/0

(l) (i) Hutumiwa kutilia mkazo maelezo/kutoa maelezo zaidi/kufafanua au kuonyesha kusisitiza. Kwa mfano:

Alinunua matunda — maembe, machungwa na matango.

(ii) Hutumiwa kuonyesha kubadilika kwa maoni. Kwa mfano:

Waite wale — hapana, hawa.

(iii) Kuonyesha msemaji/usemi halisi, kwa mfano

Utengano ni udhaifu duma

2x1 (Alama 2)

For more visit: eazyarabic.com

(m) Sentensi ibainishe kauli au hali ya kutendeana. Osore na Ngungui wamepigiana simu.

**Au**

Osore and Ngungui wamepigania simu

1x2 (Alama 2)

(n) Utumbuizaji wa Mayaka una ucheshi mwingi/sana.

**Au**

Kutumbuiza kwa Mayaka kuna ucheshi mwingi/sana.

**Au**

Kutumbuiza kwa Mayaka kuna kuchekesha kwingi/sana.

1x2 - (Alama 2)

(o) Kanda
- (i) kutomasa
- (ii) eneo
- (iii) aina ya mfuko
- (iv) mtu asiyeaminika/laghai/ayari
- (v) wingi wa ukanda/mshipi
- (vi) malipo kwa mganga
- (vii) makasia ya kuogelea
- (viii) utepe/mshipi unaotumiwa kunasia sauti/picha
- (ix) mtu asiyesimika/hanithi 3 x 1 (Alama 3)

(p)
- (i) enda mvange
- (ii) enda upogo
- (iii) enda segemnege
- (iv) enda arijojo
- (v) enda mrama
- (vi) enda benibeni
- (vii) enda shoro
- (viii) enda tenge 2 x 1 (Alama 2)

4. Isimujamii

(a) Biashara/sokoni/kunadi au kutangaza bidhaa (Alama 2)

(b)
- (i) Matumizi ya chuku - kuona ni bure, bure kwa bure, bei ya starehe
- (ii) Urudiaji - ng'ara, ng'ara, haya haya
- (iii) Matumizi ya misimu ya biashara kama vile: nguo motomoto hamsa, ng'ara,
- (iv) Lugha shawishi - shika mwenyewe ujionee, usikose mwanangu, bei nafuu
- (v) Kauli fupifupi - kuona ni bure, bei nafuu
- (vi) Lugha nyepesi - kifungu chaeleweka bila tatizo.
- (vii) Kuchanganya ndimi - *fifty fifty/Hamsa fifty*
- (viii) Matini huwa fupi. Tangazo hili ni fupi.
- (ix) Kuzungumza na mteja moja kwa moja - Haya ng'ara, usikose mwanangu.
- (x) Kutumia mafumbo ambayo huenda yasieleweke na asiyekuwa na makini. mf. Hamsa *fifty*/Hamsa na nyingine - kumaanisha mia, wala si hamsini.
- (xi) Kujinasibisha au kujitambulisha na mteja. Mtangazaji anamwita mnunuzi mwanangu ili kujenga ukuruba baina yao, hivyo kumvutia.
- (xii) Matumizi ya porojo - bure kwa bure, bei ya starehe.

8x1 alama 8

**Tanbihi**
- (i) Masharti yote ya usahihishaji wa karatasi ya pili yazingatiwe.
- (ii) Ni muhimu **mtahini** kuwa **makini** kufasiri ipasavyo majibu ya watahiniwa asije akawahini.